

MTAZAMO WA HALI YA HAKI ZA KIRAI NA KISIASA TANZANIA 2016



Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar





Shukrani

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) vinatambua mchango wa wadau mbalimbali katika kuandaa taarifa hii ya mtazamo wa hali ya haki za kiraia na kisiasa Tanzania. Tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Kitengo cha Maendeleo ya Kimataifa cha nchi ya Uingereza (DFID) kwa kufadhili mradi wa UHAKIKI ambaao mojawapo ya kazi zake ni kuandaa taarifa hii. Shukrani za pekee ziwaendee waangalizi wa haki za binadamu upande wa Tanzania Bara na wasaidizi sheria upande wa Zanzibar kwa kushiriki katika kujibu madodoso ambayo yalitumika kupata mitazamo yao na jamii zinazowazunguka kuhusu hali ya haki za kiraia na kisiasa nchini Tanzania katika mikoa wanayotoka.

Tunashukuru uongozi na wafanyakazi wa LHRC na ZLSC, wakiongozwa na Dkt. Helen Kijo-Bisimba na Bi. Harusi Mpatani, kwa ushirikiano wao katika kuandaa taarifa hii. Tunapenda kutoa shukrani kwa Wakili Imelda-Lulu Urio, Wakili Rosemary Manase, Bw. Paul Mikongoti, Bw. Fundikila Wazambi, Bw. Johnson Mbwambo, Bw. Castor Kalemera, Bw. Rodrick Maro, Bw. Majaliwa Ngailo na Bw. Denis Machui, kutoka LHRC; na Bw. Thabit Abdulla Juma, Bw. Ali Haji Hassan, na Bi. Moza Kawambwa Nzole, kutoka ZLSC kwa kushiriki kwa karibu katika kuandaa na kuandika ripoti hii. Shukrani za Kipekee ziwaendee Bw. Fundikila Wazambi na Bw. Paul Mikongoti kwa kukamilisha ripoti hii.

Pia, tunawashukuru wadau mbalimbali ambo walishiriki katika kupitia mwongozo na dodoso ambavyo vilitumika katika kuandaa ripoti hii na kutoa maoni yao. Wadau hawa ni Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP Mtandao); Chama cha Wanahabari Wanawake Tanzania (TAMWA); Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo; Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC); Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; shirika la HelpAge International; Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake (WLAC); Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG); shirika la kutetea haki za watu wenye ualbino (Under the Same Sun); shirika la Policy Forum; Baraza la Dini mbalimbali la Amani Tanzania (IRCPT); na Kituo cha Afya ya Wazee na Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi (JB Geriatric & HIV Centre).

Mwisho, tungependa kutoa shukrani zetu za dhati kwa timu ya mradi wa UHAKIKI iliyoshiriki kutoa msaada katika kuandaa ripoti hii, tukianza na Dkt. Nicole Streamlau, ambaye ni kiongozi wa timu hiyo. Wengine ni Bi. Jessica Hayes; Dkt. Linda Helgesson Sekei; Bi. Adelaide Kisinda; Bi. Dorica Andrew; na Bw. Bernard Sefu.



Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

Umewezeshwa na mradi wa UHAKIKI, ambaao upo chini ya ufadhili wa msaada wa Waingereza kutoka Serikali ya Uingereza LHRC na ZLSC ni mashirika yasiyo ya kiserikali yaliyo chini ya ufadhili wa Ubalozi wa Norway na Ubalozi wa Sweden



Yaliyomo

Shukrani	1
Muhtasari.....	3
Utangulizi: Mtazamo wa Hali ya Haki za Kiraia na Kisiasa Tanzania.....	6
Matukio Makubwa yaliyotokea Mwaka 2016	7
Mtazamo wa Haki za Kiraia na Kisiasa 2016	11
Uhuru wa Kutoa Maoni.....	11
Uhuru wa Kukusanyika.....	12
Haki ya Kupiga Kura	14
Haki ya Kuishi-Mauaji na Ukatili sababu ya Imani za Kishirikina	15
Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili mikononi mwa Vyombo vyta Dola	16
Haki ya Kuishi-Kujichukulia Sheria Mkononi.....	18
Mikoa na Haki za Kuangalia mwaka 2017.....	20
Mikoa ya kutazamwa Zaidi kwa Mwaka 2017	20
Haki za Muhimu za Kuangalia Mwaka 2017	20
Methodolojia na Alama	22
Viashiria.....	23
Alama za Mtizamo kwa Kila Mkoa	26
Bibliografia.....	27



Muhtasari

Mwaka 2016 ulinzi wa haki za msingi za kiraia na kisiasa nchini Tanzania umepata alama ya wastani ya C. Hali ya haki za kiraia na kisiasa inachukuliwa kuwa ya wastani kwa mujibu wa waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria nchini kote. Ripoti hii imechochewa na ripoti nydingine za mtazamo za kimataifa na kupelekea Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar kwa msaada wa mradi wa UHAKIKI ambao upo chini ya ufadhili wa Uingereza, kutengeneza ripoti ya awali ili kupata taarifa ya mwaka inayoangaza mambo sita kwenye haki kuu nne za kiraia na kisiasa. Alama zilizopatikana zinaweza kulinganishwa kwa mikoa na kusaidia kupata mwenendo wa hali ya haki hizo kwa miaka tofauti. Huu ni mwaka wa kwanza kwa ripoti hii kuandalliwa na inaweka msingi kwa miaka ijayo, ambapo mwenendo wa haki za kiraia na kisiasa utakokotolewa na mwenendo kujulikana.





Ripoti ya Mtazamo wa Hali ya Haki za Kiraia na Kisiasa Tanzania inatoa alama katika ngazi ya taifa na mkoa kwa mambo sita kwenye haki kuu nne. Alama hizi ni kwa mujibu wa mitazamo mtandao wa waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria nchini kote. LHRC na ZLSC zimewapa mafunzo na kuwasaidia waangalizi na wasaidizi hawa kutoka mikoa mbalimbali na wakashiriki katika ukusanyaji wa taarifa ambapo walitoa tathmini ya hali ya haki za kiraia na kisiasa katika mikoa yao. Walitoa tathmini hiyo kwa kuzingatia uzoefu wao na mtazamo katika jamii zao. Mitazamo yao imetokana na hali ilivyo katika mazingira yanayowazunguka pamoja na uelewa wao juu ya haki za binadamu.

Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, yametokea maendeleo mbalimbali makubwa, hasi na chanya ambayo yanaathiri ulinzi na utetezi wa haki za kiraia na kisiasa. Kwa mfano, Serikali ya Awamu ya Tano imefanya mabadiliko ya msingi katika kupunguza rushwa na ubadhilifu Serikalini, wakati ambapo kwa upande mwingine Serikali imehusika katika kuwekwa vikwazo kwenye haki za kiraia na kisiasa, hususani uhuru wa kukusanyika na uhuru wa kujieleza. Mchakato wa utungaji wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari uliibua mjadala na wasiwasi kuhusu uhuru wa habari nchini, huku **sheria mpya zikileta vikwazo vipyta kwenye Haki ya Kujiyeza**. Lakini pia, Serikali imekosolewa kwa **uzuiaji holela wa mikutano na mikusanyiko ya kisiasa, hatua inayozuia uhuru ya watu kukusanyika**. Hata hivyo, kumekuwa na maendeleo chanya, **hususani mwelekeo chanya wa serikali katika ulinzi wa wazee na watu wenye ualbino**. Zaidi, wakati ambapo matukio ya kujichukulia sheria mikononi yamekithiri na kuhatarisha haki ya kuishi nchini. **Suala hili limepewa mtazamo wa kitaifa likitolewa matamko na viongozi wakuu wa Serikali, akiwemo Waziri Mkuu**. Pia, wakati ambapo matukio ya mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola yakiendelea kuwa suala kubwa la uvunjifu wa haki za binadamu, tumeshuhudia **Mahakama zikishughulikia mashauri mbalimbali ya polisi walioshitakiwa kwa mauaji na ukatili kwa raia**.


Wakati ambapo katika ngazi ya kitaifa maendeleo haya yamekuwa yakitokea, yameleta athari kimtazamo katika ngazi ya mkoa. Pamoja na kuweka msingi, ripoti hii inatoa taswira hali ya sasa ya haki za kiraia na kisiasa katika mikoa yote ya Tanzania. Matokeo ya ripoti hii yanavuta hisia na ni kiashiria kwamba katika muktadha wa baada ya uchaguzi mkuu, hali ya haki za msingi za kiraia na kisiasa inaonekana kuwa mbaya hadi wastani. Hii inaonyesha haja ya kushughulikia masuala muhimu katika ngazi ya mkoa ili kuboresha hali ya haki hizi nchini.

Ripoti hii imejikita katika masuala muhimu matatu ya haki ya kuishi– mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola, kujichukulia sheria mikononi na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina, ambayo yanawaathiri wazee na watu wenye ualbino. Katika ripoti hii mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola yamepata alama D, ambayo ni alama ya chini kabisa ukilinganisha na mambo mengine ya haki za binadamu ambayo yameangaliwa katika ripoti hii. Taarifa hii inaangaza masuala muhimu na kutoa uchambuzi ambao unasaidia kufanunua utolewaji wa alama hii, kwa mfano mtazamo wa uwajibikaji wa polisi. Haki ya kuishi kwa upande wa mauaji na vurugu zinazotokana na imani za kishirikina ilipata alama C+. Ingawa kiulinganifu alama hii ni kubwa kuliko zote, alama hii ni ya wastani kitaifa, ambapo masuala ya mauaji yanayotokana na imani za kishirikina yanachukuliwa kuwa ni masuala ambayo yanaathiri mikoa mahsus, kama vile mikoa ya kanda ya ziwa. Mikoa ya ya Tabora, Songwe na Shinyanga imepata alama za chini kama mikoa iliyothirika kwa kiasi kikubwa na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina. Kwa

mwaka 2017 ripoti itajikita zaidi katika mikoa hii ili kufanya tathmini kuona kama mtazamo katika masuala haya muhimu umebadilika.

Kwa mwaka 2016, uhuru wa kukusanyika na haki ya kupiga Kura zimepata alama D+ wakati ambapo uhuru wa kujieleza umepata alama C , ambayo ni wastani. Miiongoni mwa sababu za kupata alama mbaya kwa baadhi ya haki hizi ni kutokana na kuathirika na msimamo wa Serikali wa kutokuvumilia shughuli za kisiasa baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Hii imepelekeea kupigwa marufuku kwa mikutano ya kisiasa, ya ndani na hadhara, kupigwa marufuku kwa maandamano yoyote yanayohusishwa na siasa na shughuli nyingine za kisiasa. Matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa haki ya kujieleza imepata alama C, ambayo kwa wastani ni nzuri ikizingatiwa mambo yaliyojiteze ambapo taasisi mbalimbali na watu binafsi waliitwa na kuhojiwa na mamlaka na wengine kufikiwa hadi kushitakiwa kwa kutoa mawazo ambayo yalidhaniwa kuwa yana lengo la kuchochea jamii, katika hadhara mbalimbali.

Serikali kupitia Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora pamoja na asasi za kiraia zinapaswa kuchukua hatua kutoa elimu na kuongeza uelewa wa haki za kiraia na kisiasa kwa jamii. Uhuru wa kujieleza ni dhana muhimu kwa demokrasia; na hivyo, Serikali inapaswa ihakikishe sheria muhimu kama vile Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, Sheria ya Takwimu na Sheria ya Huduma ya Vyombo vya Habari zinafanyiwa marekebisho kwa kuzingatia mapendekezo ya wadau ndani na nje ya nchi. Pale ambapo polisi wanazuia mikutano wanapaswa kutoa sababu za msingi kwa maandishi. Kwa kushirikiana na mahakama, polisi wanapaswa kuongeza kasi ya kufanya upelelezi na kuwafikisha mahakamani washitakiwa wa mauaji na ukatili dhidi ya watu wenye ualbino ili kulinda haki yao ya kuishi. Ili kukuza haki ya kuishi, Wizara ya Mambo ya Ndani itengeneze utaratibu wa kuhakikisha maafisa wa vyombo vya dola ambao wanatuhumiwa kufanya ukatili na mauaji wanachukuliwa hatua stahiki. Serikali na asasi za kiraia zihamasishe jamii kutokujichukulia sheria mkononi; polisi pia wanahitaji kuchukua hatua madhubuti kwa watuhumiwa wa uhalifu ili kurudisha imani ya jamii kwao na kupunguza matukio ya kujichukulia sheria mkononi. Hatua hizi zitasaidia kuboresha haki za msingi za kiraia na kisiasa nchini ambazo nyingi zao zimepata alama za wastani chini ya C kama ramani inavyoonyesha hapa chini.





Utangulizi: Mtazamo wa Hali ya Haki za Kiraia na Kisiasa Tanzania

Ripoti ya Mtazamo ya Haki za Kiraia na Kisiasa Tanzania ni zao la utatifiti unaofanywa kila mwaka na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC) kupitia waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria katika kila mkoa nchini Tanzania. Kupitia wangaalizi na wasaidizi hawa, LHRC na ZLSC zinaangalia mwenendo wa hali ya haki za kirai na kisiasa. Ripoti hii inatengeneza utaratibu wa kufuatilia haki hizo kuanzia ngazi ya chini, kwa kutumia ufanuzi na viashiria ambavyo wale wanaofanya uangalizi wa haki za binadamu nchini wamevivumbua katika jamii zao. Methodolojia ya ripoti hii imetengenezwa kwa kufuata mfano wa ripoti nyingine za mtazamo, lakini ikibadilishwa kuendeana na muktadha wa Tanzania.

Ripoti hii ya mtazamo imejikita katika masuala sita ya haki za kiraia na kisiasa ambayo ni; **Uhuru wa Kujiyeza; Haki ya Kupiga Kura; Uhuru ya Kukusanyika; Haki ya Kuishi kwa upande wa Mauaji na Ukatili mikononi mwa vyombo vya dola, Kujichukulia Sheria Mkononi na Mauaji Yanayotokana na Imani za Kishirikina.**

Ripoti hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza inaelezea matukio makubwa ya kijamii, kisiasa na kiuchumi yaliyotokea katika mwaka 2016, hususan baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015. Sehemu ya pili imejikita katika kuelezea matokeo ya mtazamo wa waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria, ikijumuisha mapendekezo ya namna ya kuboresha alama za haki hizi. Sehemu ya tatu imejikita katika haki na mikoa ya kuangaliwa kwa mwaka 2017, maboresho yanayoweza kufanyika, na jinsi hali ya haki za kiraia na kisiasa inavyoweza kuimarika au kudorora.

Ripoti hii inatoa matokeo ya mtazamo na uchambuzi ili kuvumbua maeneo ambayo yanaweza kuboreshwa. Kuna upungufu mkubwa wa takwimu za haki za kiraia na kisiasa nchini, kwa hivyo nia ya ripoti hii ni pia kuchangia katika uwepo wa ushahidi na uchambuzi kwa ajili ya kufanya utetezi. Ripoti ya mwaka huu inaweka msingi kwa ajili kulingalisha hali ya haki za kiraia na kisiasa kwa miaka ijayo.



Matukio Makubwa yaliyotokea Mwaka 2016

Kwa mwaka 2016, haki ya kujieleza imetia shaka zaidi kwa sababu ya vikwazo mbalimbali vilivyowekwa dhidi ya mikutano ya kisiasa. Haki hizi ziliminywa ili "kuiwezesha" Serikali kutimiza ahadi ilizotoa wakati wa uchaguzi mkuu. Haki ya kuishi imeendelea kuathiriwa na matukio ya kujichukulia sheria mikononi, mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola. Kw aupande wa Zanzibar, kufutwa kwa matokeo ya uchaguzi wa mwaka 2015 kuliibua mjadala mkubwa nchini kuhusu uhalali wa uamuzi huo.

Sheria mpya yaleta vikwazo vipyka kwenye uhuru ya kujieleza

Kwa mwaka 2015, utafiti wa shirika la *Freedom House* kuhusu uhuru ulionyesha kwamba Tanzania imeshuka katika viwango vya uhuru vya kimataifa, ikishuka toka 3.0 hadi 3.5,¹ hii ikiwa ni mara ya kwanza ndani ya kipindi cha miaka 20 kwa Tanzania kushuka katika viwango hivyo². Kushuka huku katika viwango kumesababishwa na utungwaji wa Sheria ya Takwimu na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni za mwaka 2015, ambazo 'zimeathiri kwa kiwango kikubwa utendaji wa vyombo vya habari, taasisi za kielimu na asasi za kiraia.'³ Kwa mantiki hiyo, kutungwa kwa sheria nyingine

inayominha taasisi hizi kunaweza kushuka zaidi kwa alama.

Ingawa *Freedom House* bado haijatoa matokeo ya mwaka 2016, matukio mbalimbali yaliyotokea mwaka 2016 hayaonyeshi matumaini ya haki hii kupata alama nzuri. Mwezi wa Oktoba, Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ilipitishwa na Bunge na kusainiwa na Rais kuwa sheria kamili mwezi Novemba. Kabla ya mwezi Oktoba, asasi za kiraia na wadau wengine, vikiwemo vyombo vya habari, waulipinga muswada wa sheria hii, wakitoa sababu kwamba muswada unabana haki ya kujieleza. Mionganoni mwa mambo muhimu ni pamoja na kutokuwepo kwa ulinzi wa kutosha wa uhuru wa kujieleza kwa kutohakikisha uhuru kwa vyombo vya habari na vyombo vya uratibu na usimamizi wa vyombo vya habari. Muswada huo pia ulikosolewa kwa kuminya uhuru wa habari na kujieleza kwa kuwataka waandishi wa habari wapate vibali na kuweka kigezo cha elimu. Pamoja na mambo haya yote muswada huu ulipitishwa na kuwa sheria.

Ukiacha miswada na sheria mpya, watawala walifanya vitendo mbalimbali ambavyo vinatia shaka mwaka 2016. Mionganoni mwa vitendo hivyo ni pamoja na kupiga marufuku na kulipisha faini magazeti mbalimbali na vituo vya redio. Kwa mfano, mwezi wa Januari mwaka 2016 Serikali ililifungia gazeti la *Mawio* kuchapisha na kusambaza nakala zake;⁴ na mwezi Agosti mwaka 2016 ililifungia kwa miezi mitatu Gazeti la *Mseto*⁵. Magazeti yote mawili yalifungiwa madai ya kuvunja Sheria ya

¹ Kipimo cha alama hizi ni kuanzia 1 mpaka 7, 1 ikiwa huru 'zaidi'. Kwa hivyo alama ya 3.5 ni kiwango kidogo cha uhuru kulinganisha na alama ya 3.

² Mtega Blog *Has Tanzania passed Peak Freedom is the latest Freedom House Rating a Temporary Blip?* (2016), Angalia hapa [link](#).

³ Freedom in the World 2016 – Tanzania, Angalia hapa [link](#).

⁴ Kamati ya Kulinda Waandishi wa Habari, *Tanzania yalifungia gazeti la kila wiki*, Angalia hapa [link](#).

⁵ East African, *Tanzania bans Mseto newspaper for three years*, Newspaper Article (11 Aug 2016), Angalia hapa [link](#).



Magazeti ya mwaka 1976, ambayo imekuwa ikilalamikiwa kama sheria kandamizi.

Mbali na hayo, watu mbalimbali waliitwa na kuhojiwa na polisi kwa kutoa maoni yao ambayo yalismekana na nia ya kuleta uchochezi kwa jamii. Kwa mfano, mwandishi mashuhuri nchini, Jenerali Ulimwengu, aliiitwa na kuhojiwa na polisi kwa kutoa maoni katika mdahalo wa kila mwaka uliofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Polisi walimtuhumu mwandishi huyu wa habari kwa kutoa maoni ya uchochezi kwa kumkosoa Rais mstaafu, Jakaya Kikwete.⁶

Serikali ilipata msukumo zaidi wa kuhakikisha kuwa inalinda na kuzingatia uhuru wa kujieleza kupitia kwenye Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Tathmini ya Haki za Binadamu (Universal Periodic Review). Kupitia mchakato huu Serikali ilipewa mapendekezo ya kufanya marekebisho sheria na miswada iliyopitishwa karibuni na Bunge kama vile Muswada wa Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, Sheria ya Upatikanaji wa Habari na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni ambazo zinaminyu uhuru wa kujieleza.⁷ Serikali pia ilepewa mapendekezo kuhakikisha kuwa mfumo wa kisheria na utekelezaji wa sheria hizi ambazo zinawaathiri zaidi watendaji wa vyombo vya habari zinifuata misingi ya haki za binadamu na misingi muhimu ya uhuru kama inavyohakikisha kwenye Tamko la Ulimwengu la Haki za Binadamu.⁸ Hata

hivyo, Serikali ilikataa mapendekezo haya kwa kile ilichoeleza miswada na sheria hizo iliandaliwa na kupitishwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali.⁹

Uzuiaji holela wa mikutano ya kisiasa unakiuka haki ya watu ya kukusanyika

Uhuru wa kukusanyika nayo pia ilipata misukosuko mikubwa kwa mwaka 2016. Kama ilivyooonyeshwa katika muhtasari wa LHRC na ZLSC wa kuhusu uhuru wa kukusanyika, mamlaka husika (polisi) zina uwezo wa kuzuia mikusanyiko kwa kuzingatia masharti mahsus fulani. Hata hivyo, kuna mambo ambayo hayajakaa sawa kuhusiana na mamlaka hayo ya kuzuia kwa kuwa 'mikutano inazuiwa bila kutolewa sababu za msingi, hali ambayo inapelekea kuwepo kwa shaka juu ya nia ya uzuiaji huo.'¹⁰ Mwaka 2016 Rais alitoa pendekezo la kuzuia shughuli za kisiasa hadi mwaka 2020.¹¹ Pendekezo hili lilitafsiriwa na polisi na baadhi ya viongozi wa serikali kuwa lilimaanisha kupiga marufuku mikutano ya kisiasa, ya ndani na ya hadhara.¹² Miongoni mwa mikutano mashuhuri iliyozuiwa ni ile ilioandaliwa na umoja wa vyama vya upinzani ulioitwa UKUTA. Japokuwa polisi waliondoa zuio hilo mwezi wa Septemba 2016, bado kuna mazuo holela katika baadhi ya mikoa, hali ambayo inalifanya jambo hili kuwa suala muhimu mwaka 2016.

⁶ Gazeti la *Mwananchi*, "Jenerali Ulimwengu amrushia kombora JK" (tarehe 14 Juni 2016), linapatikana kwenye [link](#).

⁷ Taarifa ya Kikundi Kazi juu ya Mpango wa Umoja wa Mataifa wa Tathmini ya Haki za Binadamu kwa Tanzania, "Views on conclusions and/or recommendations, voluntary commitments and replies presented by the State under review", ukurasa wa 2 hadi 4, inapatikana [link](#).

⁸ Ibid

⁹ 8

¹⁰ Ibid

¹¹ LHRC na ZLSC (2015), *Muhtasari wa Mada:Uhuru wa kukusanyika ni Haki ya Kiraia*

¹² IPP Media, "Mafuriko ya kisiasa marufuku hadi 2020" inapatikana [link](#).

¹² Gazeti la *The Citizen*, "No agreement on legality of ban of meetings, (26 Agosti 2016), linapatikana [link](#).



Asasi za kiraia zimeendele kuweka shinikizo kwa Serikali kutekeleza na kulinda uhuru wa kukusanyika, ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo mbalimbali wakati wa mchakato wa tathmini ya haki za binadamu (*Universal Periodic Review*) lakini kuna ishara ndogo ya Serikali kuyafanya kazi mapendekezo hayo. Viongozi wa kidini waliomba kukutana na Rais kwa ajili ya kuzungumzia maendeleo ya hali ya kisiasa nchini. Ombi hilo halijapata majibu mpaka sasa.¹³

Mwenendo chanya wa Serikali kuchukua hatua kuwalinda wazee na watu wenye ualbino

Kwa mwaka 2016 Serikali imechukua hatua muhimu kubadilisha mtazamo wa watanzania kuhusu wazee, watu wenye ulemavu na watu wenye ualbino. Miongoni mwa hatua hizi chanya ni pamoja na kuteuliwa kwa Dk. Abdallah Possi, ambaye ni mtu mwenye ualbino, pamoja na Ndugu Amoni Mpanju, ambaye ni mtu asiyiona, kwenye nafasi za juu za serikalini. Kwa upande wa Zanzibar nako pia watu wawili wenye ulemavu waliteuliwa kwenye Baraza la Wawakilishi. Hatua nyingine za kupongezwa zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na ziara mbalimbali zilizofanywa na viongozi wa juu wa serikali kwenye vituo vya kulelea wazee na watu wenye ulemavu; lakini pia na uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuamua kuwalipa pensheni ya mwezi wazee wa Zanzibar kwa ajili ya kujikimu. Hatua hizi ni viashiria kuwa juhudzi zinafanywa kulinda haki ya msingi

kabisa ya kuishi kwa makundi haya muhimu maalum.

Maamuzi ya Mahakama dhidi ya mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola, ila matamko ya kutia shaka yanayochocha mauaji hayo

Pamoja na kuwa na matukio chanya kama yalivyoonyesha hapo juu haki ya kuishi bado ipo hatarini wakati ambapo matukio ya vurugu yamekuwa hayashughulikiwi. Polisi wanatakiwa kufuata taratibu pale wanapokuwa wanawashughulikia watuhumiwa wa uhalifu mbalimbali. Hata hivyo, kwa mwaka 2016 kumekuwa na mifano mbalimbali ambapo viongozi wa Serikali wametoa matamko mbalimbali ambayo yanakumbatia – na labda pia kuchocha – ukatili mikononi mwa vyombo vya dola. Kwa mfano, mwezi Agosti mwaka 2016 Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam alinukuliwa akiwahimiza polisi watumie nguvu zinazoweza kusababisha mauti dhidi ya watuhumiwa wa mauaji ya polisi. Kauli hiyo aliitoa wakati wa mazishi ya askari polisi waliouawa kufuata shambulizi lililofanywa kwenye kituo kimojawapo cha polisi mwezi Agosti mwaka 2016 jijini Dar es Salaam.¹⁴ Kauli hii inaleta hatari ya askari polisi kutumia nguvu kupita kiasi wakati wa kuwashughulikia washtakiwa wa uhalifu, hali ambayo inaweza kusababisha mauaji ya washitakiwa hawa.

Pamoja na kuwa kauli ya Mkuu wa Mkoa inaonyesha kukuzwa kwa kwa matumizi ya kupindukia ya nguvu, kumekuwa pia na

¹³ Gazeti la *Mwananchi*, "Sakata la Ukuta:Viongozi wa dini wasota kumuona Rais" (23 Novemba 2016), linapatikana [link](#).

¹⁴ *Angalia* Tamko kwa Vyombo vya habari lililotolewa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora likikosoa kauli iliyo tolewa na Mkuu wa Mkoa, linapatikana [link](#); *angalia* pia Ayo TV, VIDEO:'Polisi mkimkuta mtu kwenye msitu piga, haki za binadamu waje kwangu'- RC Makonda, at [link](#).



mambo chanya yaliyohusisha mahakama, yakionyesha kwamba mahakama inafanya juhudzi za kulinda haki ya kuishi dhidi ya mauaji na vurugu mikononi mwa vyombo vya dola. Mwaka 2016 kulikuwa na hukumu mbili zilizotolewa na mahakama dhidi ya askari polisi walioshitakiwa kwa mauaji ya raia. Mojawapo ya hukumu hizo inamuhusisha askari polisi ambaye alihusika kwenye mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi, ambapo mshitakiwa alihukumiwa kwa kuua bila kukusudia na kwenda jela kwa miaka 15. Hukumu nyingine ilimuhusisha askari polisi wa cheo cha juu ambaye alishitakiwa kwa kuhusika katika mauaji ya wafanyabiasha wa jijini Dar es Salaam mnamo mwaka 2002, ambapo askari huyo alihukumiwa adhabu ya kifo.

Pamoja na kuwa na kuwepo kwa mambo haya chanya bado kuna matatizo ya suala la uwajibikaji wa polisi na hatua zinazochukuliwa dhidi ya vitendo hivi kama inavyoonyeshwa katika kadi ya matokeo ya taarifa hii.

Ajenda ya matukio ya kujichukulia sheria mikononi imefanywa kuwa ya kitaifa

Jambo jingine la msingi lililotoka mwaka 2016 ni suala la kujichukulia sheria mikononi kuchukuliwa kama tatizo la kitaifa na si kimkoa tena. Mwaka 2016 kulitoka mauaji ya watafiti yanayodaiwa kufanywa na kikundi cha wanakijiji huko Dodoma.¹⁵ Tukio hili lilichukua sura ya kitaifa na kupelekeea kitendo hiki kukemewa nchi nzima. Washutumiwa wa kitendo hiki cha

kujichukulia sheria mikononi walialaaniwa nchini kote, wakakamatwa na kushtakiwa mahakamani kwa kitendo hicho. Mauaji haya ya kikatili yalipelekea Waziri Mkuu kuamrisha kukamatwa kwa wote walioshutumiwa kuhusika na mauaji hayo. Jeshi la Polisi na asasi za kiraia pia zilishutumu vikalivitendo kama hivyo vya wananchi kujichukulia sheria mikononi.

Hitimisho

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu hii, haya ndio yamekuwa matukio makubwa kuhusiana na haki za kiraia na kisiasa yaliyotokea mwaka 2016 ambayo yamekua yakiathiri ulinzi na ukuzaji wa haki za kiraia na kisiasa. Sura inayofuata ya taarifa hii itachambua matokeo ya utafiti, na kutilia mkazo mitazamo muhimu katika mikoa mbalimbali ya hali ya haki za kiraia na kisiasa katika ngazi ya chini kabisa ya jamii. Sehemu hii itaweka msingi muhimu kwa ajili ya uchambuzi wa mwenendo wa hali ya haki za kiraia na kisiasa kwa siku za mbele.


¹⁵ *Angalia Gazeti la the Citizen*, "Shock over slaying of Arusha researchers" (2 Oktoba 2016) linapatikana [link](#).

Mtazamo wa Haki za Kiraia na Kisiasa 2016

Uhuru wa Kutoa Maoni

Pointi (wastani) = 3.2, Alama=C

Kwa mwaka 2016, hali ya uhuru wa kutoa maoni nchini Tanzania ilionekana kuwa ya wastani, ikipata alama C.¹⁶ Alama hii ni kubwa kiasi ukilinganisha na alama za haki na masuala mengine matano ambayo yameangaliwa katika ripoti hii. Hata hivyo, chati hapo chini inaonyesha kuwa japokuwa mikoa mingi imepata alama za wastani, ni mkoa mmoja tu ndio ulipata alama juu ya C+. Pia, matukio mbalimbali katika ngazi ya kitaifa yanatia shaka na kuna hatari ya alama hii kushuka mwaka ujao ikiwa uhuru wa kutoa maoni utaendelea kuwekewa vikwazo na athari zake kufikia katika ngazi ya mkoa.



Kwa mwaka 2016, hali ya uhuru wa kutoa maoni mkoa wa Dar es Salaam (alama B) inaonekana ni nzuri, wakati ambapo mikoa mingine imepata alama za juu kidogo ya wastani, alama C+, kama vile mikoa ya Tanga, Kigoma,

Simiyu na Mwanza (miongoni mwa mikoa mingine mingi).

Kuna sababu mbalimbali ambazo zimechangia mikoa hii kupata alama za juu kuliko mikoa mingine. Hii ni pamoja na mtazamo kwamba kwa ujumla Serikali inaruhusu wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru, ikiwemo yale yanayohusu siasa. Sababu nyingine ni pamoja na mtazamo kwamba wanawake wanaongea kwa uhuru katika sehemu mbalimbali. Japokuwa mkoa wa Dar es Salaam umepata alama ya juu kiasi, ilionekana kwamba uhuru wa watumishi wa umma kutoa maoni kuhusu masuala ya kisiasa umeminywa sana. Hili lilionekana katika mikoa mingi.

Mikoa iliopata alama ya chini zaidi ni pamoja na Songwe, Tabora na Kusini Pemba yote ikiwa imepata alama D. Katika mikoa hii zilitajwa sababu kuu zilizosababisha mikoa hii kupata alama za chini. Sababu hizi ni pamoja na watumishi wa umma kutokuwa huru kuongea kuhusu masuala ya kisiasa na ufahamu mdogo kuhusiana haki za msingi za binadamu, ikiwemo uhuru wa kutoa maoni. Pia, waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria katika mikoa hii walitaja sababu nyingine kuwa wanawake kutoshiriki vyta kutosha katika mikutano na baadhi ya mila na desturi kuwanyima au kuminya nafasi zao za kutoa maoni na kelezea masuala yanayowagusa. Uhuru wa vyombo vyta habari ultajwa kama tatizo katika mikoa hii, wanahabari na vyombo vyta habari vikipata changamoto kutoa habari kutokana na vikwazo mbalimbali.

¹⁶ Angalia sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



Mikoa iliyopata alama za juu

Dar es Salaam	B	4
Tanga	C+	3.9
Kigoma	C+	3.8
Niombe	C+	3.7
Manyara	C+	3.6
Simiyu	C+	3.6
Mwanza	C+	3.6
Morogoro	C+	3.5

Mikoa iliyopata alama za chini

Kusini Pemba	D	2.3
Songwe	D	2.1
Tabora	D	2.1

Kuna uwezekano wa alama ya uhuru wa kutoa maoni kuongezeka mwaka ujao kama masuala muhimu yanayoathiri uhuru wa wananchi kutoa maoni yao katika ngazi za kitaifa na kimkoa yatafanyiwa kazi, hasa katika mikoa iliyopata alama za chini. Uhuru wa kutoa maoni ulikua ni sababu kuu iliyochangia kupata alama za juu katika mikoa iliyopata alama hizi. Hata hivyo hata katika mikoa hii uhuru wa watumishi wa umma kutoa maoni yao kwa uhuru unaonekana kuwa unaminywa. Hivyo, kulinda uhuru wa kutoa maoni katika sekta ya utumishi ni muhimu na suala la msingi kwa Serikali kuliangalia mwaka 2017.

Japokuwa kuona matokeo mazuri kutachukua muda, Serikali na asasi za kiraia zinatakiwa kufanya juhudzi zaidi kuongeza uelewa kwa wananchi kuhusu umuhimu wa wanawake kushiriki na kushirikishwa katika kutoa

maamuzi katika jamii na kuhakikisha uhuru huo wa kutoa maoni unakuzwa na kulindwa.

Katika muhtasari wao kuhusiana na uhuru wa kutoa maoni uliotolewa hivi karibuni, LHRC na ZLSC wametoa mapendekezo mbalimbali ambayo yamewalenga watunga sera katika ngazi ya taifa.¹⁷ Mapendekezo hayo yamelenga vikwazo vyta uhuru wa maoni vilivyowekwa na sheria mpya. Mapendekezo haya bado yana umuhimu kwa kuwa athari ya sheria hizo mpya bado zinaonekana katika ngazi ya mkoa, ambapo uhuru wa vyombo vyta habari umetajwa kama mojawapo ya mambo yanayoathiri mikoa iliyopata alama za chini. Serikali inatakiwa kuzipitia upya na kuzifanya marekebisho sheria hizi, ambazo ni Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, Sheria ya Takwimu na Sheria ya Huduma ya Vyombo vyta Habari, ambazo zimekosolewa ndani na nje ya nchi.


Uhuru wa Kukusanyika

Pointi (wastani) = 2.8, Alama = D+

Katika kipindi hiki cha baada ya uchaguzi Mkuu wa Oktoba mwaka 2015, uhuru wa kukusanyika umeonakana kuwa hauko vizuri, ukipata alama ya D+.¹⁸ Kama ilivyoelezewa hapo juu, kumekuwa na hali yenye kutia wasiwasi mwaka 2016, hali ambayo imepelekea kuwepo mtazamo kwamba Serikali inazuia mikusanyiko bila sababu za msingi. Matokeo ya utafiti kwa mwaka 2016 yanaonyesha kwamba zaidi ya nusu ya mikoa (asilimia 55) ilipata alama za D na F (alama za chini), kama ambavyo chati inaonyesha hapa chini.

¹⁷ Angalia LHRC na ZLSC (2016), Muhtasari: Uhuru wa Kujieleza. Unapatikana katika ofisi za LHRC na katika tovuti zao.

¹⁸ Angalia sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



Kwa mwaka 2016 hakuna mkoa uliopata alama juu ya C+ kwenye uhuru wa kukusanyika. Mikoa ya Simiyu, Tanga, Lindi, Iringa na Morogoro ilipata alama ya juu kuliko mikoa mingine, yote ikipata alama C+.

Wakati hali ya mikoa hii inaonekana kuwa juu kidogo ya wastani, kuna mambo kadhaa yaliyochangia kupata alama za juu zaidi kuliko mikoa mingine katika mikoa hii. Mambo hayo ni pamoja na mtazamo kwamba polisi wanatoa ulinzi kwenye mikusanyiko na mamlaka na watumishi wa serikali hawaingilii au kuzuia mikutano, ikiwemo ya kisiasa.

Ripoti inaonyesha alama mbaya sana katika mikoa ya Tabora na Shinyanga. Mikoa mingine, kama Songwe na Ruvuma, imepata alama nzuri kidogo lakini bado hali katika mikoa hii pia inaonekana kuwa mbaya. Mionganoni mwa sababu zilizotajwa kusababisha alama ndogo katika mikoa hii ni pamoja na mtazamo kwamba polisi hawatoi ulinzi kwenye mikusanyiko kwa usawa na wanawabughudhi waandaji wa mikusanyiko husika. Sababu nyingine iliyotajwa ni ubaguzi unaofanywa na mamlaka za serikali za mtaa katika kutoa vibali vya maeneo za kufanya mikutano.

Wakati waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria wakiona uhuru wa kukusanyika katika mikoa kama Simiyu na Tanga unaingiliwa kidogo, kwa ujumla uhuru huu unaonekana kuwa katika hali mbaya nchini Tanzania.

Mikoa iliyopata alama za juu

Simiyu	C+	3.8
Tanga	C+	3.6
Lindi	C+	3.6
Iringa	C+	3.6
Morogoro	C+	3.6

Mikoa iliyopata alama za chini

Arusha	D	2.4
Kusini Unguja	D	2.4
Dar es Salaam	D	2.4
Pwani	D	2.4
Kaskazini Pemba	D	2.2
Mara	D	2.2
Kusini Pemba	D	2.2
Ruvuma	D	2
Songwe	D	2
Tabora	F	1.8
Shinyanga	F	1.4

Kutakuwa na matumaini ya uhuru huu kupata alama ya juu zaidi kwa mwaka 2017 ikiwa masuala muhimu yatafanyiwa kazi katika ngazi ya taifa na mkoa. Kuna mapendekezo kadhaa ambayo asasi za LHRC na ZLSC zimeyatoa kwenye muhtasari wao kuhusu haki hii ya uhuru wa



kukusanyika, ambayo ni mabsusi kwa polisi na Serikali.¹⁹ Katika ngazi ya mkoa na wilaya, polisi wanatakiwa kutumia vizuri na kwa ueledi mamlaka yao ya kuzuia mikusanyiko chini ya Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma Saidizi bila upendeleo wowote. Polisi pia wanatakiwa kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa salama wanapokuwa wanafurahia haki yao ya kukusanyika, kwa kutoa ulinzi wa kutosha. Na pale ambapo mkusanyiko umezuiwa, basi polisi watoe sababu za msingi na kwa maandishi. Mambo haya ni ya msingi katika kulinda haki hii, na yataleta athari katika ngazi za mkoa na taifa. Mapendekezo haya yasipofanyiwa kazi alama ya haki hii itabaki kuwa mbaya, au hata kuwa mbaya zaidi (F) mwaka 2017.


Haki ya Kupiga Kura

Pointi (wastani) = 2.9, Grade = D+

Kwa mwaka 2016, Haki ya Kupiga Kura imepewa alama D+ na waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria.²⁰ Mitazamo yao imejikita zaidi kwenye uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, hali ilivyokuwa baada ya uchaguzi huo, na marudio ya uchaguzi wa Zanzibar mwaka 2016.

Mwaka wa 2016 Mikoa ya Geita, Simiyu na Morogoro ni mikoa pekee iliopata alama C. Mambo kadhaa yamechangia kupata alama hizi, ikiwemo utoaji wa elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura uliofanywa na Serikali na asasi za kiraia na mtazamo kwamba wanahabari

wako huru kutoa taarifa na kuandika kuhusu uchaguzi na kampeni za uchaguzi. Mambo mengine ni mtazamo kwamba wanahabari na vyombo vya habari vimekuwa havibughudhiwi na kuingiliwa; na mtazamo kwamba kwa kiasi kikubwa wanawake wako huru kushiriki katika chaguzi na kuwapigia kura wagombea wanaowataka; na pia watu wenye ulemavu kuweza kushiriki kwenye mchakato wa uchaguzi.



Kwa upande mwingine, kuna mikoa ambayo imepata alama za chini, kama Mkoa wa Songwe ambao ulipata alama ya kufeli (F) wakati mikoa ya Lindi na Shinyanga imepata alama D. Katika mikoa hii, alama za chini zinatokana na mtazamo kwamba elimu ya uraia na mpiga kura haikupatikana maeneo mengi, pamoja na vyombo vya habari kuwa na ubaguzi katika kutoa taarifa kuhusu vyama vya siasa. Ilionekana pia kwamba wanahabari na vyombo vya habari havikuwa huru kutoa taarifa ndani ya mikoa hii wakati wa uchaguzi. Mambo mengine ambayo yaliibuliwa ni pamoja na wanawake kutushiriki kwa uhuru katika siasa na uchaguzi (mfano kupigia kura viongozi wanaowapenda na kugombea nafasi za uongozi) na watu wenye ulemavu kutopewa msaada wa kutosha kuwawezesha kushiriki

¹⁹ Angalia LHRC na ZLSC (2016), *Muhtasari: Uhuru wa kukusanyika ni Haki ya Kiraia*. Unapatikana katika ofisi za LHRC na ZLSC, pamoja na tovuti zao.

²⁰ Angalia sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



katika uchaguzi. Sababu nyingine ni wasimamizi wa uchaguzi (NEC na ZEC) katika ngazi za mkoa na wilaya kuonekana kutofanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa na maafisa wa Serikali katika ngazi hizo na kitaifa.

Mikoa iliyopata alama za juu

Geita	B	4
Simiyu	C+	3.7
Morogoro	C+	3.7

Mikoa iliyopata alama za chini

Pwani	D	2.4
Singida	D	2.2
Tabora	D	2.1
Lindi	D	2
Shinyanga	D	2
Songwe	F	1.3

LHRC na mtandao wa asasi za kiraia wa uangalizi wa uchaguzi wa TACCEO wamegusia mambo mbalimbali ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi katika taarifa yao ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.²¹ Taarifa hii imetoa mapendekezo muhimu mbalimbali, ambayo baadhi yake yameshaanza kufanyiwa kazi, ikiwemo zoezi la elimu ya uraia na mpiga kura kuwa endelevu kuanzia mwaka 2017. Mapendekezo mengine in pamoja na vyombo vya habari kutoa taarifa za uchaguzi bila upendeleo wowote na kwa

ueledi. Ili alama ya haki ya kupiga kura ipande katika miaka ijayo, mambo haya inabidi yafanyiwe kazi na kuleta athari katika ngazi ya mkoa. Hatua ya Serikali kuamua kuendelea na elimu ya uraia mpaka kufikia uchaguzi ujao ni nzuri na inaweza kusababisha alama ya haki hii kupanda katika miaka ijayo.

Haki ya Kuishi-Mauaji na Ukatili sababu ya Imani za Kishirikina

Pointi (wastani) = **3.7**, Alama = **C+**

Kwa mwaka 2016 haki ya kuishi kwenye upande wa mauji na ukatili yanayosababishwa na imani za kishirikina ilipata alama C+, hii ikionyesha kwamba waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria wanaona suala hili lipo juu kidogo ya wastani, ambao ni C.²² Hata hivyo, alama hii ya wastani inajumuisha alama nzuri zilizotolewa kwa mikoa ambayo mauaji haya na ukatili huu huwa hayatokei au nadra sana kutokea, mfano Dar es Salaam, Mtwara, na Kaskazini Unguja. Katika mikoa hii wajazaji wa dodoso walieleza kwamba hakuwa na taarifa ya matukio ya mauaji na ukatili kama huo mwaka 2016 na Serikali ina mahusiano mazuri na waganga wa jadi.


Hata hivyo, kuna mikoa ambayo matukio ya mauji na ukatili sababu ya imani za kishirikina yameonekana kutoa sana, **ikiwemo Songwe, Tabora, na Shinyanga ambayo yote imepata alama D kwa mwaka 2016**; na hii ni kutokana na upelelezi mbovu unaofanywa

²¹ LHRC na TACCEO (2016), *Taarifa ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015*

²² Angalia sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



na polisi dhidi ya watuhumiwa wa mauaji na ukatili huo, kesi kutoendeshwa kwa umakini na uharaka mahakamani, na watu wenye ualbino kutohisi wapo salama. Mambo mengine yaliyotajwa katika mikoa iliyopata alama za chini ni pamoja na uhusiano mbovu kati ya Serikali na waganga wa jadi na wataalamu wa tiba mbadala, pamoja na ubaguzi wa watu wenye ulemavu na wazee kwenye familia na jamii zao.



Kwa mwaka wa 2017 taarifa hii itaiangalia mikoa hii iliyopata alama za chini kuona kama mtazamo umebadilika na alama kupanda au la. Ili mikoa hii ipate alama za juu zaidi lazima mambo ambayo yamesababisha ipate alama za chini yashughulikiwe moja kwa moja. Kwa mfano, vyombo vya polisi na mahakama vinatakiwa kuchunguza na kuendesha mashtaka kwa ueledi na uharaka. Mapendekezo haya yamekuwa yakitolewa mara kwa mara, na yalitolewa pia na LHRC katika taarifa yake ya haki za binadamu ya mwaka 2015.²³ Pia, kuna haja ya polisi na jamii kwa ujumla kuongeza juhudhi katika kutoa ulinzi kwa watu wenye ualbino na wazee. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iingize haki za watu wenye

ualbino na wazee kwenye mitaala ya shule. Asasi za kiraia na taasisi za serikali kama vile Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora zitoe elimu na kueneza ufahamu kuhusu haki ya kuishi kwenye haya maeneo.

Mikoa iliyopata alama za juu

Mtwara	A	5
Kaskazini Pemba	B+	4.9
Kusini Unguja	B+	4.9
Dar es Salaam	B+	4.9
Kusini Pemba	B+	4.8

Mikoa iliyopata alama za chini

Shinyanga	D	2.4
Songwe	D	2.3
Tabora	D	2.3


Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili mikononi mwa Vyombo vya Dola

Pointi (wastani) = 2.4, Alama = D

Kwa mwaka 2016, haki ya kuishi inaonekana kuhatarishwa na mauaji na ukatili mikononi mwa vyombo vya dola, ikipata wastani wa alama ndogo kuliko zote katika haki za kiraia na kisiasa zilizoangaliwa kwenye ripoti hii. Kwa mtazamo wa waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria, haki hii haijapewa ulinzi wa kutosha na hivyo kupata alama D, ambayo ni mbaya.²⁴

²³ LHRC (2015) *Tanzania Human Rights Report*, p. 38-39

²⁴ *Angalia* sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



Mikoa iliyopata alama za juu
Mikoa iliyopata alama za kati
Mikoa iliyopata alama za chini

Japokuwa alama ya haki hii ni mbaya kwa ujumla wake, kuna mikoa ambayo imepata alama nzuri, mfano **Kaskazini Unguja, ambayo umepata alama B na Simiyu, ambayo umepata alama C+**. Mtazamo katika hii mikoa ni kwamba wananchi wanalindwa wakiwa chini ya ulinzi wa polisi na wanaotoa taarifa za matukio ya uhalifu wa vyombo dola pia wanalindwa kwa utambulisho wao kuwa siri. Pia kuna mtazamo kwamba kwa ujumla kuna uchunguzi mzuri wa matukio ya mauaji na ukatili mikononi mwa vyombo vya dola.

Hata hivyo, mikoa hii ndio pekee imepata alama nzuri, **mikoa mingine 25 (asilimia 81) ikipata alama za F hadi D+, chini ya wastani**. Mikoa ya **Tabora, Songwe, Kigoma, Dar es Salaam, Mbeya na Singida ilipata alama F**. Alama hizi za chini zimesababishwa na mambo muhimu kadhaa, kama vile matukio ya polisi kufanya ukatili na kutumia nguvu kupita kiasi wakati wa kukamata watu wanaohisiwa kufanya uhalifu, muda mwingine kusababisha kifo. Uchunguzi mbovu unaofanywa na polisi kuhusiana na matukio hayo pia ultajwa kama sababu, pamoja na wanaotoa taarifa za mauaji na ukatili mikononi mwa vyombo vya dola na mashahidi kutolindwa utambulisho wao.

Mikoa iliyopata alama za juu

Kaskazini Unguja	B	4.4
Simiyu	C+	3.6
Mjini Magharibi	C	3.2
Kusini Unquia	C	3.2
Arusha	C	3
Geita	C	3

Mikoa iliyopata alama za chini


Dar es Salaam	F	1.8
Singida	F	1.8
Mbeya	F	1.6
Songwe	F	1.4
Kigoma	F	1.4
Tabora	F	1.2

Ili alama za mikoa hii ipande kwa mwaka ujao, mambo ya msingi lazima yaangaliwe, hasa kukosekana kwa utaratibu wa kushughulikia makosa na mwenendo wa maafisa wa vyombo vya dola. Utaratibu huu lazima uanzishwe, na unaweza kujumuisha kutengeneza chombo huru maalumu cha kuangalia utendaji kazi wa polisi, kama kile kilichopendekezwa kwenye Rasimu ya Pili ya Katiba, ambacho kitafanya uchunguzi na kuwawajibisha maafisa wa polisi ambao wamejihuisha na mauaji au ukatili.

Haki ya Kuishi-Kujichukulia Sheria Mkononi

Pointi (wastani) = 3, Alama = C

Kwa mwaka 2016, haki ya kuishi kwa upande wa matukio ya kujichukulia sheria mkononi umepata alama C.²⁵ Kuna mikoa ambayo imepata alama za juu kiasi, na kuna mikoa mingine imepata alama za



chini, kiashiria cha kutokuwa na usalama katika ngazi ya jamii.

Kati ya mikoa ambayo imepata alama za juu na wastani ni pamoja na Simiyu, ambayo imepata alama B; na

Iringa, Ruvuma, na Kaskazini Unguja, ambayo yote imepata alama C+.

Sababu zilizochangia kupata alama hizi ni pamoja na mtazamo kwamba viongozi wa kidini na kimila katika mikoa hii wana jukumu la kusuluhiha migogoro, hivyo kuwafanya wananchi kutoamua kujichukulia sheria mkononi mara kwa mara. Pia, katika mikoa hii mahakama zinaonekana kuchukua hatua dhidi ya wanaojichukulia sheria mkononi.

Katika Mkoa wa Simiyu, utaratibu wa kitamaduni wa kushughulikia migogoro

unaoneakana kusaidia kupambana na uhalifu. Utafiti zaidi unahitajika kuangalia ni kwa kiasi gani utaratibu huu unasaidia kutatua migogoro, ila kwa mujibu wa waangalizi wa haki za binadamu, vyombo hivi vyta kutatua migogoro vinavyojulikana kama "Dagashida" vimesaidia katika kupambana na uhalifu na kuwapa adhabu wahalifu, na hivyo kupunguza matukio ya wananchi kujichukulia sheria mkononi katika kupambana na uhalifu. Japokuwa vyombo hivi vimesaidia Simiyu kupata alama ya juu, kuna utata juu ya vyombo hivi na nafasi yake katika jamii inahitaji kuchunguzwa zaidi. Kumekuwa na taarifa za adhabu ambazo zimekuwa zikitolewa na vyombo hivi ambazo zinakiuka haki za binadamu. Kitu kingine kilichochangia Simiyu kupata alama kubwa kimetajwa kuwa ni kazi inayofanywa na Kamanda wa sasa wa Polisi wa mkoa huo. Kwa mujibu wa waangalizi wa haki za binadamu, kamanda huyo amekuwa mstari wa mbele katika kupambana na uhalifu na kurudisha kwa kiasi fulani imani ya wananchi juu ya jeshi la polisi. Mfano huu unaonyesha njia ambazo zinaweza kutumika kushughulikia tatizo la kujichukulia sheria mkononi katika ngazi ya mkoa.

Kwa upande mwingine, kuna mikoa ambayo imepata alama za chini sana, ikiwemo Dar es Salaam na Morogoro, ambayo yote imepata alama ya kufeli (F). Mikoa mingine ambayo ilipata alama za chini kiasi ni **Songwe, Singida na Tabora, yote ikipata alama D.** Mojawapo ya mambo yaliyosababisha mikoa hii kupata alama za chini ni mtazamo kwamba polisi hawawachukulii hatua watuhumiwa wanaojichukulia sheria mkononi. Ilielezwa kwamba mara nyingi polisi huchelewa kuchukua hatua pale ambapo raia wema wanapiga simu kuwaita eneo la tukio na wakati mwingine huwa wanaunga mkono

²⁵ *Angalia* sehemu inayofuata kuhusiana na viashiria, ambayo inaonyesha orodha ya viashiria kwa kila haki



vitendo vya kujichukilia sheria mkononi, hasa pale mhusika anapokuwa mtuhumiwa wa wizi. Hii imechangia wananchi kutokuwa na imani na jeshi la polisi na mfumo mzima wa haki, ambao kwa ujumla unaonekana kukumbwa na kashfa za rushwa, kwa mujibu wa tafiti mbalimbali za masuala ya rushwa za hivi karibuni.²⁶

Kutokuwa na imani na jeshi la polisi kunaonekana kuwa tatizo katika mikoa yote, hata ile iliyopata alama za juu. Kazi inayofanywa na viongozi wa kidini na kimila imesaidia kushughulikia tatizo la kujichukulia sheria mkononi.

inatakiwa kuhakikisha kwamba polisi wanachukua hatua dhidi ya wanaojichukulia sheria mkononi ili kurudisha imani ya wananchi kwa jeshi la polisi. Viongozi wa kidini na kijamii wanatakiwa watumie nafasi zao kukemea vitendo vya kujichukulia sheria mkononi. Asasi za kiraia zinaweza zikaongezea kwenye juhudini za serikali kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu madhara ya kujichukulia sheria mkononi.

Mikoa iliyopata alama za juu

Simiyu	B	4
Ruvuma	C+	3.6
Iringa	C+	3.6
Kaskazini Unguja	C+	3.6

Mikoa iliyopata alama za chini

Tabora	D	2.4
Singida	D	2.2
Songwe	D	2.2
Morogoro	F	1.8
Dar es Salaam	F	1.6

Ili kupambana na vitendo vya kujichukulia sheria mkononi, Serikali na asasi za kiraia lazima zifanye kazi kwa ukaribu pamoja na viongozi wa kijamii kushughulikia sababu zinazosabaisha wananchi kujichukulia sheria mkononi. Wizara ya Mambo ya Ndani

²⁶ *Angalia Taarifa ya Hali ya Rushwa Tanzania kwenye tovuti* [link](#) (mara ya mwisho kuangaliwa mwezi Oktoba 2016)



Mikoa na Haki za Kuangalia mwaka 2017

Mikoa ya kutazamwa Zaidi kwa Mwaka 2017

- Simiyu na Kaskazini Unguja:**
Mikoa hii imepata alama za juu zaidi katika matokeo ya mtazamo kuhusu haki za kiraia na kisiasa, hasa kwa upande wa haki ya kuishi. Kama mikoa hii itashughulikia chamngamoto kwenye uhuru wa kujieleza, uhuru wa kukusanyika na haki ya kupiga kura basi kuna uwezekano mkubwa wa kuendelea kuongoza nchini kwa kuheshimu haki za kiraia na kisiasa. Mwaka ujao tutaangalia kama mikoa hii itaendelea kupata alama za juu ya wastani au kama hali itaonekana kuwa inakuwa mbaya na kwa nini.
- Songwe, Tabora na Shinyanga:**
Mikoa hii ilipata alama za chini zaidi ukilinganisha na mikoa mingine yote. Mikoa yote miwili ilikuwa na alama za chini sana kwenye uhuru ya Kukusanyika na haki ya kuishi-mauaji na ukatili mikononi mwa vyombo vya dola. Kama kutafanyika maboresho, kuna uwezekano wa alama hizi zikaboreka na kuwa za juu kadri mwaka unavyokwenda, lakini kama serikali za mikoa zitaendelea kuminya uhuru wa kukusanyika, kushughulikia mauaji yanayotokana na imani za kishirikina na matukio ya kujichukulia sheria mikononi, basi itakua ngumu kupata mwenendo chanya.
- Morogoro, Arusha na Manyara:**
Ingawa mikoa hii imepata alama

nzuri kiasi, kuna uwezekano mkubwa wa alama hizi kushuka mwaka unaokuja kwa sababu ya kuongezeka kwa migogoro ya ardhi ambayo inaweza kupelekea watu kujichukulia sheria mkononi au mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola. Kuna uhitaji wa haraka wa kusuluuhisha migogoro ya ardhi ili kuhakikisha alama hizi zinaongekeza badala ya kupungua.

Haki za Muhimu za Kuangalia Mwaka 2017

- Haki ya Kuishi-Kujichukulia Sheria Mkononi:**
Ukizingatia alama za chini ilizopata mikoa kama Dar es Salaam na Morogoro, ambayo kwa sehemu kubwa ni mijini, kuna haja ya polisi na viongozi kurudisha imani ya wananchi juu yao ili kupunguza matuko ya kujichukulia sheria mkononi. Alama hizi zinaweza kuongezeka kwa uhalifu kushughulikiwa ipasavyo na wanaojichukulia sheria mikononi kushtakiwa, hasa katika maeneo ya mijini.
- Uhuru wa Kutoa Maoni:** Athari ya Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari zitakuwa ni za muhimu sana kufanyiwa uchambuzi kwa mwaka 2017 hasa kwa kuwa uhuru wa vyombo vya habari umeelezwa kuwa mionganini mwa matatizo katika mikoa iliyopata alama za chini. Ukizingatia shinikizo ndani nan je ya nchi, itakuwa muhimu kuangalia kama Serikali itayafanya kazi mapendekezo ya watetezi wa haki za



binadamu ya kurekebisha vipengele
vya sheria hiyo vinavyominya haki.
Itakuwa muhimu pia kufuatilia
mijadala na majadiliano kuhusu
sheria zinazoathiri mitazamo na
utendaji katika ngazi za mikoa.

- **Uhuru wa Kukusanyika:** Tumeshuhudia zuijio la mikutano na mikusanyiko ya kisasa kwa mwaka 2016, kitendo ambacho kimepelekeea mtazamo kwamba uhuru wa kukusanyika imeminywa. Japokuwa Jeshi la Polisi baadae liliondoa zuijio hilo, kitendo hicho kiliendelea kuathiri mtazamo kuhusu uhuru wa kukusanyika. Mwaka 2017 utakuwa mwaka muhimu kuangalia zuijio na vikwazo kwenye uhuru wa kukusanyika na ni kwa kiasi gani wananchi wataona wanaweza na na kukusudia kufurahia uhuru huu.
- **Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili sababu ya Imani za Kishirikina:** Taarifa ya nusu mwaka ya hali ya haki za binadamu ya 2016 inayotolewa na LHRC ilionyesha kuwa tangu mwezi Januari mpaka mwezi Juni mwaka 2016 kulikuwa na matukio ya mauaji yanayohusishwa na imani za kishirikina 394, ambayo ni ongezeko kubwa ukilinganisha na idadi ya matukio 57 yaliyopotiwa kwa kipindi kama hicho mwaka 2015. Hata hivyo, kumekuwa na viashiria chanya kwamba Serikali inachukua hatua dhidi ya matukio haya na hasa namna jamii inavyowatazama watu wenye ualbino. Kwa hiyo mwaka 2017 itakuwa muhimu kuangalia kama hatua hizi za serikali zinaleta matokeo yoyote chanya hasa katika maeneo yaliyoathirika zaidi na mauaji

haya kwa kupungua kwa mauaji na kuongezeka kwa mashtaka ya watuhumiwa wa mauaji haya kutapelekea kuboreka kwa mwenendo wa haki hii.

- **Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili Mikononi mwa na Vyombo vya Dola:** Matukio ya mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola yamechangia kwa kiasi kikubwa kushusha alama za haki katika mikoa mingi. Haki hii kwa upande wa vyombo vya dola imepata alama mbaya au mbaya zaidi kutoka kwa waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria, hii ikimaanisha kwamba ni ambalo linatakiwa kuangaliwa vizuri kitaifa. Japokuwa kumekuwa na ongezeko la mashtaka ya mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola, ikiwemo askari polisi wawili kukutwa na hatia ya mauaji hivi karibuni, kauli na matamko mbalimbali za viongozi wa serikali ambazo zinaweza kuchochaea mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola zinaweza kuwa na athari hasi kwenye alama za haki hii mwaka 2017. Kauli hizo kwa bahati mbaya zimekuwa nyingi kiasi katika miezi ya hivi karibuni, ikiashiria kwamba hatutaona ongezeko kubwa la alama ya haki hii. Miongoni mwa vitu muhimu vya kuangalia ni nafasi ya Mahakama katika kushughulikia kesi zinazotolewa mbele yake pia kauli zinazotolewa na viongozi wa serikali.



Methodolojia na Alama

Kwa mwaka 2016 utafiti wa mtazamo kuhusu hali ya haki za kiraia na kisiasa nchini Tanzania ulifanyika katika mikoa yote (Tanzania Bara na Zanzibar). Wajazaji wa madodoso walikuwa ni waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria, ambao walichaguliwa kwa kuangalia ufahamu wao katika mikoa wanayotoka na taarifa wanazotoa kwa niaba ya LHRC na ZLSC, pamoja na ujuzi wao kwenye masuala ya haki za binadamu. Jumla wa wajazaji wa madodoso 31 walihusika katika zoezi la kukusanya taarifa ambapo kila mmoja alipewa dodoso moja na kutoa alama kwenye viashiria vya kila haki kwa kutoa alama A, B, C, D au F kama zinazotumika katika mfumo shule nchini Tanzania katika ngazi za elimu ya msingi na sekondari. Wataalamu hawa walitakiwa pia kutoa maelezo kuhusiana na alama waliyotoa kwa kila kiashiria, yakielezea ni kwa nini wametoa alama hiyo. Alama walizotoa zilipitiwa na kuangaliwa wakati wa mkutano wa mapitio ambao uliwhusisha waangalizi na wasaidizi wa kisheria wote walioshiriki kwenye zoezi la kujaza dodoso na waandaji wa taarifa hii toka ZLSC na LHRC.²⁷ Dodoso lilikuwa na jumla ya viashiria 45; na liligawanya katika sehemu kuu sita kwa kila haki iliyotazwa katika utafiti huu.

Katika kuchambua takwimu na taarifa zilizopatikana, LHRC na ZLSC walikokotoa wastani wa kila haki na mkoa kwa kutumia alama zifuatazo:

Alama	A	B+	B	C+	C	D+	D	F
Wigo	5	4.5-4.9	4-4.4	3.5-3.9	3-3.4	2.5-2.9	2-2.4	1-1.9

LHRC, ZLSC na timu ya UHAKIKI walikutana na wadau mbalimbali toka serikalini na asasi nyininge za kiraia, ikiwemo Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (CHRAGG); Jeshi la Polisi; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Watoto na Wazee; *Twaweza*; shirika la kutetea haki za watu wenyewe ualbino la Under the Same Sun; na Mtando wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THDRC), wakati wa maandalizi ya utafiti na kutengeneza methodolojia. Wadau hawa walipata wasaa na nafasi ya kutoa mapendekezo kuhusiana na maswali ambayo yaliulizwa kwenye dodoso na muonekano mzima wa taarifa hii.

²⁷ Thamani za alama ni kama ifuatavyo: A (Nzuri sana) = 5; B (Nzuri) = 4; C (Wastani) = 3; D (Mbaya) = 2; na F (Feli) = 1. Alama hili zilitolewa kwa kila kiashiria, ikifuatiwa na maelezo au sababu za kutoa alama husika.



Viashiria

Waangalizi wa haki za binadamu na wasaidizi wa kisheria waliombwa kuchambua na kuweka alama kwenye haki kulingana na maelezo yaliyooanishwa na haki hizo kwa mikoa yao husika wanakofanya uangalizi na kutoa usaaidizi wa kisheria. Maelezo ya ziada yaliongezwa katika kila maelezo makuu kwa ajili ya waangalizi na wasaidizi wa kisheria wote na yanweza kupatikana pale yatakapohitajika kutoka LHRC.

Viashira vya Uhuru wa kukusanyika

- Ushiriki kwenye mikutano uko huru na salama
- Mikutano inafanyika kujadili hata mambo ambayo ni nyeti (mfano mijadala katiba, kashfa kubwa za rushwa nk)
- Polisi wanatoa ulinzi sawa katika mikutano yote
- Maeneo ya kufanya mikutano yanatolewa kwa waandaaji wote bila ya kujali itikadi ya kisiasa au mambo yanayojadiliwa ya mukutano
- Maofisa wa serikali hawaingilii uhuru wa kukusanyika

Viashiria vya Uhuru wa Kutoa Maoni

- Waandishi wa habari na wadau wengine wa habari wanaweza kufanya kazi zao kwa uhuru ndani ya mkoa kwa mujibu wa sheria na kanuni
- Mtu yejote au kundi la watu wana uhuru wakuanzisha chombo cha habari
- Watumishi wa umma wanashiriki kujadili masuala ya kisiasa kwa uwazi
- Wanawake wanapewa haki na fursa sawa za kushiriki na kuzungumza kwenye mikutano ya maamuzi ya kijamii
- Watu wenyewe ulemavu wanapewa haki na fursa sawa ya kushiriki, kuzungumza, kuelezea mawazo yao na kufanya maamuzi kwenye mikutano ya kijamii
- Watu wanaweza kujieleza na kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ya kisiasa, kijamii au kiuchumi bila kubughudhiwa au vitisho
- Wananchi wana uhuru wakushiriki kwenye mijadala ya kidini
- Viongozi wa kidini wanaweza kushiriki kwenye mijadala ya kisiasa na kijamii
- Wasanii na wanajamii wako huru kuelezea fikra zao kuitia kazi zao za sanaa
- Vyombo vya habari viko huru dhidi ya udhibiti ; rasmi au usio rasmi



Viashiria vya Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili sababu ya Imani za kishirikina

- Polisi wanashughulikia kesi za ukatili dhidi ya wazee na watu watu wenye ualbino
- Viongozi wa kimila na viongozi wa serikali za mitaa wanaingilia kati dhidi ya watu wanaowadhuru au kuwaua wazee na watu wenye ualbino
- Mahakama zinatoa hukumu kwa washtakiwa waliowadhuru au kuwaua wazee na watu wenye ualbino
- Watu wenye ualbino na wazee wako salama kushiriki shughuli za kijamii kwenye maeneo yao
- Watu wenye ualbino wana fursa sawa ndani ya familia
- Mamlaka za serikali (Serikali Kuu na Serikali za Mitaa) zinapigania na kutetea haki za ulinzi wa watu wenye ualbino na wazee wanaotuhumiwa kwa ushirikina
- Polisi wanashughulikia kesi za ukatili dhidi ya wazee wanaotuhumiwa kwa uchawi
- Viongozi wa kimila na wa serikali za mitaa wanaingilia kati dhidi ya watu wanaowajeruhi au kuwaua wazee wanaotuhumiwa kwa uchawi
- Mahakama zinatoa adhabu kwa wale wanaoshtakiwa na kukutwa na hatia ya kutenda makosa ya ukatili na mauaji dhidi ya wazee waliootuhumiwa uchawi
- Mamlaka za serikali zinawaunga mkono waganga wa kienyeji waliosajiliwa tu

Viashiria vya Haki ya Kupiga Kura

- Elimu ya mpiga kura na uraia inatolewa kwa watu wote
- Wananchi wanapata taarifa kutoka vyombo vya habari (radio, televisiuni, au magazeti) zinazoonyesha mitazamo ya makundi mbalimbali ya kisiasa
- Vyombo vya habari na waandishi wa habari wako huru kutoa taarifa za chaguzi
- Wanawake wako huru kushiriki katika mchakato wa uchaguzi bila ya vikwazo (katika kuchagua na kuchaguliwa)
- Watu wenye ulemavu hawakabiliwi na vikwazo vya mchakato wa kupiga kura (kupiga kura au kupigiwa kura)
- Taasisi za kusimamia uchaguzi ziko huru, hazibughudhiwi kisiasa
- Mchakato unaohusu upigaji kura, ujumlishaji na utangazaji wa matokeo ya uchaguzi uko huru dhidi ya vitendo vya rushwa
- Mchakato wa uchaguzi uko huru dhidi ya vitisho, unyanyasaji au vurugu
- Mchakato wa uchaguzi unaendeshwa kwa uwazi na uhuru
- Mchakato wa Uchaguzi unafikiwa na wananchi wote wenye sifa



Viashiria vya Haki ya Kuishi – Kujichukulia Sheria Mkononi

- Polisi wanashughulikia kesi zinazohusu kujichukulia sheria mkononi
- Wananchi wanaamini kuwa malalamiko kuhusu vurugu, wizi n.k yatashughulikiwa na polisi kwa haki na kwa ufanisi
- Wananchi wanaamini kuwa malalamiko yao kuhusu vurugu, wizi nk, yatashughulikiwa na viongozi wa kimila, wazee au viongozi wa dini
- Viongozi wa kijamii hawatetei, kusaidia au kuunga mkono vurugu za kujichukulia sheria mkononi
- Mahakama inatoa adhabu kwa makosa ya watu kujichukulia sheria mkononi

Haki ya Kuishi – Mauaji na Ukatili mikononi mwa Vyombo vya Dola

- Wananchi wanalindwa dhidi ya ukatili na mauaji wawapo mikononi mwa vyombo vya dola
- Polisi wanachunguza kwa ufanisi kesi za ukatili au mauaji ya wananchi/raia wakiwa mikononi mwa vyombo vya dola kama zilivyo kesi nyingine
- Mahakama zinashiriki katika uchunguzi kwa ukamilifu kesi zinazohusu ukatili na mauaji yanayofanywa na vyombo vya dola
- Kuna njia za wazi na zenye ufanisi za kufikisha malalamiko kuhusu ukatili na mauaji yanayohusishwa na vyombo vya dola
- Wananchi wanajiamini na wanajiona wako salama wanapotoa taarifa kuhusiana na vurugu au mauaji yanayotokana na watu kujichukulia sheria mkononi



Alama za Mtizamo kwa Kila Mkoa

Ufunguo:

- FoE** = Uhuru wa Kujieleza; **FoA**= Uhuru wa Kukusanyika; **RV**= Haki ya Kupiga Kura; **RLW**= Haki ya Kuishi-Mauji na Ukatili sababu ya Imani za Kishirikina; **RLE**= Haki ya Kuishi-Mauji na Ukatili mikononi mwa Vyombo vya Dola; **RLM**= Haki ya Kuishi-Kujichukulia Sheria Mkononi
- A & B** = **Juu/Nzuri**; **C** = **Wastani**; and **D & F** = **Chini/Mbaya**

Jedwali hapo chini linaonyesha mikoa na alama iliyopata kwa kila haki pamoja na alama ya wastani kwa haki zote kwa kila mkoa.

Mkoa	Alama							Mkoa	Alama						
	FoE	FoA	RV	RLW	RLE	RLM	Average		FoE	FoA	RV	RLW	RLE	RLM	Average
Simiyu	C+	C+	C+	C+	C+	B	C+	Mjini Magharibi	D+	C	D+	B	C	D+	C
Kaskazini Unguja	C	C	C	A	B	C+	C+	Morogoro	C+	C+	C+	C	D+	F	C
Tanga	C+	C+	D+	B	D	C	C	Dar es Salaam	B	D	C	B+	F	F	C
Arusha	C	D	C	B	C	C	C	Kagera	C	D+	D+	D+	D	D+	D+
Mtwara	D+	D+	D+	A	D	C	C	Dodoma	D+	D+	C	D+	D+	D+	D+
Mwanza	C+	C	C	C	D	C	C	Lindi	D+	C+	D	B	D	D+	D+
Geita	C+	C	B	C+	C	C	C	Manyara	C+	D+	D+	C	D	C	D+
Iringa	C	C+	C	C+	D+	C+	C	Mara	C	D	D+	C	D+	C	D+
Katavi	C	C	C	C	D	C	C	Mbeya	D+	D+	C	C	F	C	D+
Kigoma	C+	C	C	C+	F	C	C	Singida	C	D+	D	C+	F	D	D+
Kilimanjaro	C	C	D+	C+	D+	C	C	Pwani	D+	D	D	D+	D+	C	D+
Kusini Pemba	D	D	D+	B+	D+	C	C	Rukwa	C	C	D+	C+	D	D+	D+
Kusini Unguja	C	D	D+	B+	C	D+	C	Shinyanga	D+	F	D	D	D	D+	D
Njombe	C+	C	C	C+	D	D+	C	Tabora	D	F	D	D	F	D	D
Kaskazini Pemba	C	D	C	B+	D	C	C	Songwe	D	D	F	D	F	D	F
Ruvuma	C	D	C	C	D+	C+	C								



Bibliografia

Ayo TV (2016) *Polisi mkimkuta mtu kwenye msitu piga, haki za binadamu waje kwangu'*- RC Makonda, Video 25 Aug. 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Business anti-corruption portal (2016) *Tanzania Corruption Report*. Inapatikana kwemye tovuti: [link](#). (mara ya mwisho kuangaliwa Oktoba 2016)

Commission for Human Rights and Good Governance (CHRAGG) (2016)
Taarifa kwa vyombo vya habari Press Statement 26 Aug 2016. Available online: [link](#).

Committee to Protect Journalists (2016) *Tanzania imposes ban on weekly newspaper* CPJ Online Alert. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Freedom House (2016) *Freedom of the Press 2016*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Freedom House (2016) *Freedom in the World 2016 – Tanzania*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Friedrich Ebert Stiftung (2015). *The African Media Barometer*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

HABARILEO (2016), *Majaliwa awalaani walioua watafiti*. Makala kwenye Gazeti, 5 Oktoba 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

IPP Media (July 2016), *Mafuriko ya kisiasa marufuku hadi 2020*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Legal and Human Rights Centre (LHRC) (2016) *Tanzania Human Rights Report 2015: Tanzania Mainland* Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

LHRC (2016) *Thematic Briefing: Freedom of Expression*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

LHRC and Tanzania Civil Society Consortium For Election Observation (TACCEO) (2016) Report on the United Republic of Tanzania General Elections of 2015 Report. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

LHRC and ZLSC (2015) *Thematic Brief - Freedom of Assembly is a Civil Right*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Mtega Blog (2016) *Has Tanzania passed "peak freedom"? Or is the latest Freedom House rating a temporary blip?* Blog post: 8 Feb 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Mwananchi (2016) *Sakata la Ukuta: Viongozi wa dini wasota kumuona Rais*. Newspaper Article (23 November 2016). Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Mwananchi (2016) *Jenerali Ulimwengu amrushia kombora JK*. Newspaper Article 14 June 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

The Citizen (2016) *No agreement on legality of ban of meetings*. Newspaper Article 26 Agosti 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

The Citizen (2016) *Shock over slaying of Arusha researchers*. Newspaper Article 2 Oct 2016. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Transparency International (2015) *Corruption Perceptions Index*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).

Working Group on the Universal Periodic Review (2016) *Report of the Working Group on the Universal Periodic Review: United Republic of Tanzania*. Inapatikana kwenye tovuti: [link](#).



Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar

